

Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2026 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2026.

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 11-20 MEI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilisababisha ukanda mvua kuendelea kuwepo katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani, na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Aidha, mifumo ya hali ya hewa iliyopo katika ukanda wa ziwa Victoria kuimarika pamoja na upepo wa bahari wenye unyevunuevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani viliendelea kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2026.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria na vipindi vya mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2026.

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua kuendelea kuwepo katika maeneo ya kanda wa ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani, na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2026.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Hali ya ukavu inatarajiwa.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Imetolewa na:

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz